

Athari za Kinyarwanda katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili katika Shule Teule za Sekondari Wilayani Gakenke, Rwanda

Martin H. Ikuramutse¹, Vivens Niyotugira² na Pascal Sebazungu³

Ikisiri

Makala hii inachunguza jinsi Kinyarwanda kinavyoathiri ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili. Watoataarifa 24 ambaa ni wanafunzi 18, walimu 3 pamoja na wakuu wa masomo 3, walitumiwa kuwa vyanzo vyaa taarifa. Data hizo zilikusanya kuitia mahojiano, ushuhudiaji pamoja na udurusu wa nyaraka. Nadharia ya Utibia ilioasisiwa na Skinner mwaka 1950 ndiyo ilioongoza utafiti huu. Matokeo yanaonesha kwamba wanafunzi wanachanganya Kinyarwanda na Kiswahili kwa kuwa lugha hizi zina mfanano wa karibu kimatamshi, kiotografia na kisemantiki. Hivyo basi, makala hii inapendekeza yafuatayo: mosi, kuwe na vitabu vyaa ziada na kiada shulenii. Pili, ufundishaji wa Kiswahili uwe wa lazima kuanzia shule za chekechea hadi vyuoni. Tatu, Kiswahili kifundishwe katika michepoo yote kama ilivyo kwa lugha ya Kiingereza. Mwisho, kuwe na mijadala na midahalo shulenii ili kuboresha kiwango cha lugha ya Kiswahili mionganii mwa wanafunzi.

1.0 Utangulizi

Katika dunia mamboleo, ujuzi wa lugha zaidi ya moja umekuwa kitu muhimu maishani. Kutohakana na umuhimu huo, serikali ya Rwanda ilianzisha ufundishaji wa lugha za kigeni katika mfumo wake wa elimu. Mionganii mwa lugha zilizoanza kufundishwa ni Kiswahili. Lugha ya Kiswahili ilianza kufundishwa rasmi nchini Rwanda kwenye shule zake mwaka 1979 (Mlaga, 2017). Mambo haya yote yalifanyika kulingana na mkataba uliosainiwa baina ya Serikali ya Rwanda na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kuanzia wakati huo, Kiswahili kilikubaliwa

¹Mhadhiri Msaidizi, Idara ya Lugha, Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Kabgayi, Rwanda. Baruapepe: ikuramabert@gmail.com

² Mwanafunzi wa Shahada ya Umahiri wa Kiswahili katika Elimu, Ndaki ya Elimu, Chuo Kikuu cha Rwanda. Baruapepe: niyotugiravivens@gmail.com

³ Mwanafunzi wa Shahada ya Umahiri wa Kiswahili katika Elimu, Ndaki ya Elimu, Chuo Kikuu cha Rwanda. Baruapepe: psebazungu@gmail.com

japo mwaka 2017 ndipo hasa kilikubaliwa kuwa lugha rasmi nchini Rwanda. Mbali na hayo, uainishaji wa lugha za Kibantu uliofanywa na Malcom Guthrie unaonesha kuwa Kinyarwanda huhesabiwa katika kundi la JD (Maho, 2009). Lugha hii huwaunganisha na kuwatambulisha Wanyarwanda kupitia utamaduni wao kama lugha ya taifa na wanaitumia nchini kote bila tafsiri yoyote. Rwanda hutumia lugha nne rasmi ambazo ni Kinyarwanda (lugha ya taifa), Kiingereza, Kifaransa na Kiswahili. Idadi kubwa ya wazungumzaji wa lugha ya Kinyarwanda huonekana katika Afrika ya Kati kwenye Ukanda wa Maziwa Makuu wa Afrika Wazungumzaji hao hutoka katika nchi zinazopakana na Rwanda, yaani Uganda (Kaskazini), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mashariki), Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (Magharibi) na Burundi (Kusini). Mtaala mpya uliotangazwa na Wizara ya Elimu, kupitia Bodi ya Elimu ya Rwanda kwa shule za sekondari mwaka 2015 ulilazimisha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili. Jambo hili lilifanyika kutoka kidato cha kwanza hadi cha tatu ambapo Kiswahili kinafundishwa vipindi viwili kwa wiki. Kwa upande mwingine, lugha hii inafundishwa kutoka kidato cha nne hadi cha sita. Katika vidato hivyo kuna vipindi sita kwa wiki. Ijapokuwa lugha husika hufundishwa katika vipindi hivyo, ujuzi wa wanafunzi ungali uko katika kiwango cha chini. Hali hii inasababishwa na ujifunzaji wa Kiswahili katika mazingira ya Kinyarwanda. Mbali na hayo, ingawa serikali ya Rwanda iliweka jitihada kubwa katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili, bado kuna changamoto zinazokabili ufundishaji wa lugha hii. Niyomugabo (2016) anabainisha kuwa wanafunzi wa Kinyarwanda wanaonekana kuzoea kuzungumza Kinyarwanda mahali popote walipo. Mazoea hayo hutokea wakiuliza na kujibu maswali kwa Kinyarwanda badala ya kutumia Kiswahili. Pia, mazoea haya hujitokeza wanapowasiliana wao kwa wao. Hivyo basi, mwingiliano huo unaoanishwa na maoni ya Debyser (1970). Maoni ya mtaalamu huyu yanasema kuwa mwingiliano wa lugha huweza kujitokeza kama ajali ya lugha mbili ambayo husababishwa na kukutana kwa lugha hizo. Aidha, Debyser (1970) anaonesha kuwa mwingiliano wa lugha unaegemea kwenye viwango vya kitamaduni na kiisimu, kama vile fonetiki, mofosintaksia na leksikosemantiki. Viwango hivi huathiriwa na lugha ya kwanza ambayo hujitokeza mara nyingi kwa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili.

Naye Ntawiyanga (2016) amebainisha kuwa wanafunzi hufanya makosa ya upatanisho wa nomino na vivumishi, upatanisho wa kiwakilishi kirejeshi cha nomino na upatanisho wa nomino na kitenzi. Mtaalamu huyu anaendelea kubainisha kuwa makosa hayo hutokana na athari za lugha ya kwanza ingawa mengine hutokana na kujumuisha kanuni za Kiswahili ili kujirahisishia ujifunzaji. Mbali na hayo, inaonekana kuwa wanafunzi hawaimudu lugha ya Kiswahili kama ilivyo kwani makosa hayo hukwamisha malengo ya ufundishaji na ujifunzaji. Kimenyi (2003),

Ntawigira (2011) pamoja na Ntawiyanga (2015) walionesha kuwa ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika muktadha wa Rwanda hukumbwa na changamoto mbalimbali zinazostahili kufanyiwa utafiti ili kutoa suluhisho mwafaka. Kwa hivyo, makala hii imechunguza athari za Kinyarwanda katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili.

2.0 Mapitio ya Maandiko kuhusu Athari za Lugha ya Kwanza kwa Lugha ya Pili
 Lugha ya kwanza hufunzwa katika mazingira ya familia badala ya mazingira ya shuleni na hufunzwa kiasili huku lugha ya pili ikifunzwa katika mazingira ya shule na mwezeshaji. Mara nyingi, mtu anayejifunza lugha ya pili huwa na tabia ya kutumia muundo wa sentensi au sarufi ya lugha yake ya kwanza katika lugha ya pili. Mwalimu anaweza kurejelea lugha mama ili kuthibitisha kwamba wanafunzi wameelewa kile kilichokuwa kikifundishwa. Matumizi ya lugha ya kwanza katika kufundisha lugha ya pili ni suala ambalo limejadiliwa katika tafiti mbalimbali. Ellis (1994) anafafanua kwamba lugha ya kwanza inaweza kuwa kizuizi katika kujifunza lugha ya pili. Hali hii inatokana na kuingiliana kwa lugha, hofu ya kufanya makosa au kuendelea kuwa na mawazo katika lugha ya kwanza.

Matumizi ya lugha ya kwanza yanayo julikana kama ya lazima katika mchakato wa ufundishaji, yanakatazwa kutumika katika darasa la lugha ya pili ili kuepuka tabia ya hasira kwa wanafunzi inayosababishwa na kuitumia lugha yao ya kwanza. Katika uwanja wa ufundishaji wa lugha ya kigeni, wataalamu pamoja na walimu wana wasiwasi kuhusu matumizi ya lugha ya kwanza katika darasa la lugha ya kigeni. Hata hivyo, umilisi wa lugha ya kwanza humsaidia mwanafunzi kujifunza lugha ya pili. Hivyo basi, uzoefu wa wanafunzi katika lugha mama unahamasishwa kwenye lugha ya pili kwa lengo la kujifunza lugha lengwa (Richards, 1974).

Tafiti za mwanzo zilionesha nafasi ya lugha ya kwanza katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili. Ngugi (2007) anabainisha kuwa lugha ya Kikuyu huathiri ujifunzaji wa Kiswahili katika kiwango cha kifonolojia. Utafiti wake ulibainisha kuwa matamshi ya wanafunzi pamoja na tahajia ndivyo vinavyoathiriwa zaidi. Sio hayo tu, Ngugi (*keshatajwa*) anaeleza kwamba makosa mengi hutokana na udondoshaji na uchopekaji wa irabu. Hata hivyo, utafiti huu uliegemea katika fonolojia bila kuchunguza viwango vingine vya isimu. Nao Fromkin, Rodman na Hyman (2007) wanaeleza kuwa wanafunzi wa lugha ya pili hufanya makosa ya uhamishaji wa sarufi ya lugha ya kwanza kwenda lugha ya pili. Watafiti hawa wanabainisha kuwa makosa mengi hudhihirika katika viwango vya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia. Wanaismu hawa wanatoa mfano wa Mjapani ambaye anajifunza lugha ya Kiingereza pale anaposhindwa kutofautisha *write* (andika) na *light* (mwanga). Hali hii inatokana na kuwa sauti r na 1 hazimo katika lugha yao kwanza. Kutokana na maelezo hayo,

tunaona kuwa viwango vya fonolojia, mofolojia na sintaksia huathiriwa zaidi kuliko viwango vingine pale wanafunzi wanapojifunza lugha ya pili.

Utafiti wa Komunte (2001) kuhusu athari za lugha za Kibantu katika kujifunza Kiingereza mionganoni mwa wanafunzi wa shule za upili nchini Tanzania unadhihirisha kwamba wanafunzi wote wamezoea kutumia lugha za Kibantu ndani ya darasa. Uchunguzi wake ulieleza kwamba 82.9% ya wanafunzi wanafikiria kwanza katika lugha ya kwanza na baadaye kuwasilisha istilahi husika katika lugha ya Kiingereza pale wanapojifunza stadi za kusoma na kuzungumza. Mtafiti huyu anabainisha pia kuwa idadi kubwa ya wanafunzi haina umilisi wa lugha ya Kiingereza kwa kuwa wanatamka maneno mengi ya lugha hiyo kama yanavyoandikwa. Utafiti huu unatuonesha kuwa lugha ya kwanza huchangia zaidi katika matamshi yasiyo sahihi.

Kwa mujibu wa Ontieri (2017), athari za kifonolojia za lugha teule za Kibantu katika Kiswahili hujitokeza katika udondoshaji, uchopekaji na ubadilishaji wa fonimu. Udondoshaji hudhihirika katika insha za wanafunzi wa Kikuyu. Makosa hayo yalioneckana kwenye sauti nazali pamoja na sauti mwambatano. Udondoshaji ni mabadiliko ya sauti ambayo hutokea wakati wa kuunda maneno kwa muktadha wa lugha fulani. Hii inaweza kujumuisha kubadilika kwa sauti fulani au herufi kutoka neno moja hadi lingine, mara nyingi kwa sababu ya mabadiliko ya kihistoria au kanuni za sarufi ya lugha hiyo. Kwa mujibu wa Ontieri (2010), maneno yanayodhihirisha kasoro ni pamoja na *uAgedhani* badala ya *ungedhani*, *majoAzi* badala ya *majonzi*, *kiwaAja* badala ya *kiwanja*, *kuvuAja* badala ya *kuvunja*. Mifano hii inaonesha kuwa nazali /n/ ilidondoshwa na kuathiri maneno husika.

Mtaalamu huyu anaendelea kubainisha kuwa uchopekaji hudhihirika mionganoni mwa wanafunzi wazawa wa Kikuyu katika insha walizoiandika. Sauti nazali /n/, /m/ na irabu /u/ zilijitokeza kwa wingi katika uchopekaji. Yafuatayo ni baadhi ya maneno yalioathiriwa zaidi: *inje* badala ya *nje*, *kumuwacha* badala ya *kumwacha* na **mbumbuazi** badala ya *bumbuazi*. Irabu *i* ilichopekwa mwanzoni mwa neno *nje* kwa njia isiyo sahihi. Neno *kumuwacha* linaonesha namna irabu /u/ ilivyochopekwa katikati ya konsonanti *m* na *w*. Pia, konsonanti **m** ilichopekwa mwanzoni mwa neno *bumbuazi* na kuleta kasoro katika neno husika. Ubadilishaji wa fonimu ultokea katika insha za wanafunzi wazawa wa lugha ya Kikuyu. Fonimu kama vile /r/ na /l/ zilibadilishana nafasi ifuatayo: kukabiriana badala ya kukabiliana, serikari badala ya serikalⁱ na tulijaribu badala ya tulijaⁱlibu. Wanafunzi wazawa wa Kikuyu wanatumia /r/ badala ya /l/ kwani hawana sauti /l/ katika lugha yao. Hivyo, wanatumia sauti ambayo wanaifahamu, yaani /r/ na kusababisha kasoro katika maneno insha.

Sio hayo tu, utafiti wa Ontieri (*keshatajwa*) ulihu pia lugha ya Kikisii na kubainisha athari za lugha hiyo katika ubadilishaji wa fonimu na kuleta kasoro. Yafuatayo ni baadhi ya maneno yaliyoathiriwa: msindo badala ya **mshindo**,

kushugulika badala ya kushughulika, anayechincha badala ya anayechinjwa. Hivyo basi, mifano hiyo inaonesha jinsi ambavyo wanafunzi walitumia /s/ badala ya /ʃ/, /g/ badala ya /s/ na /f/ badala ya /ʃ/. Ukweli ni kwamba fonimu hizo hazipo katika lugha ya Kikisii, hivyo kumfanya mwanafunzi atumie /s/, /g/ na /f/ ambazo hupatikana katika lugha ya Kikisii. Matumizi ya fonimu hizi huathiri ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa ujumla. Kwa hivyo, makala hii inaongeza maarifa mionganoni mwa wataalamu wa Kiswahili katika kuona athari zinazojitokeza kwenye ufundishaji wa Kiswahili katika muktadha wa Rwanda, hasa katika lugha za Kibantu.

3.0 Methodolojia na Misingi ya Kinadharia

Methodolojia na misingi ya kinadharia ni muhimu katika utafiti kwa sababu huwezesha mtafiti kuchagua mbinu zinazofaa, kuelezea matokeo kwa usahihi na kuhakikisha utafiti una uhalali na uwazi. Mbinu hizi zinatoa mwongozo wa kisayansi unaosaidia kujenga hoja madhubuti na kudumisha ubora wa utafiti. Kwa hiyo, sehemu hii inajadili kwa kina methodolojia na nadharia iliyotumika katika makala hii.

3.1 Methodolojia ya Utafiti

Utafiti huu umefanyika wilayani Gakenke, mkoani Kaskazini, nchini Rwanda. Watoataarifa walikuwa walimu watatu wa Kiswahili, wanafunzi kumi na wanane pamoja na wakuu wa masomo watatu katika shule teule. Mbinu za usampulishaji zisizo nasibu na lengwa zilitumika katika kuwachagua watoataarifa wote. Walimu na wanafunzi waliteuliwa kutokana na kuwa na umilisi wa lugha ya Kiswahili na sifa za ufundishaji na ujifunzaji. Vilevile, data za utafiti zilikusanya kwa njia ya ushuhudiaji darasani, mahojiano pamoja na udurusu wa nyaraka. Njia hizi ziliwawezesha watafiti kukusanya data za kuaminika kuhusu athari za Kinyarwanda katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili. Aidha, mikabala ya kitaamuli na kitakwimu ilitumika katika kuchambua na kuchanganua data za utafiti huu. Mkabala wa kitaamuli unatumwiwa kuchambua na kuchanganua data kwa njia ya maeleo bila matumizi ya takwimu (Ponera, 2019).

Hivyo basi, data za ushuhudiaji zilipatikana pale watafiti walipoingia darasani na kushuhudia kitendo cha ufundishaji lugha huku wakiongozwa na mwongozo wa ushuhudiaji. Njia ya mahojiano ilifanywa na watafiti ana kwa ana kwa watoataarifa wote ambao walijibu maswali yaliyoandikwa kwenye karatasi yaliyolenga athari za Kinyarwanda katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili. Shule zilizoteuliwa ni pamoja na ES. Nyacyina, College Methodiste Uni de Rushashi (CMUR) na GS. Kirebe. Shule hizo zinafanana kwa msingi kwamba zote zipo kwenye maeneo ya vijijini.

Wanafunzi wa kidato cha nne kwenye shule ya kwanza husoma lugha ya Kiswahili kama somo linalotahiniwa katika mtihani wa taifa. Pia, wanafunzi hawa ndio walioanza kuisoma lugha hii kwenye mkondo wa lugha nchini Rwanda. Tuliwahoji wanafunzi wa kidato cha sita kwenye shule ya pili kwani wana msingi mpana wa kutumia Kiswahili wakiwa katika maandalizi ya kufanya mtihani wa taifa. Pia, wanafunzi hao wanatarajiwa kutumia lugha ya Kiswahili kwenye ajira zao na katika kutatua changamoto za kijamii. Shule ya tatu ilikuwa na wanafunzi wanaosoma lugha ya Kiswahili kama somo la hiari. Tuliwahoji wanafunzi wa kidato cha pili kwani wana msingi kwenye lugha ya Kiswahili kwa sababu walikuwa wametimiza miaka miwili tangu walipoanza kusoma Kiswahili.

3.2 Misingi ya Kinadharia

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Utibia ambayo ni nguzo muhimu katika kufundisha lugha ya pili. Nadharia ya Utibia iliyoasisiwa na F.B. Skinner miaka ya 1950, inadai kuwa mwanafunzi hujifunza lugha kwa kurudiarudia. Bichwa na Mwendamseke (2021) wanabainisha kuwa Nadharia ya Utibia inaongozwa na mihimili mitatu ambayo ni uzoeshi, uimarisho chanya na uimarisho hasi. Vilevile, Nadharia ya Utibia hutathminiwa katika tabia za wanafunzi ambazo huonekana katika vitendo kulingana na malengo yaliyokusudiwa. Kwa mujibu wa Bichwa na Mwendamseke (*weshatajwa*), mwalimu humpa mwanafunzi kichocheo na jibu au matokeo ya mwanafunzi kulingana na kichocheo ambacho huaminika kama mwitiko. Kwa hiyo, kichocheo ni aina ya ufundishaji na ujifunzaji inayotolewa na mwalimu na mwitiko ni athari au tabia inayopimwa au kuonekana kwa mwanafunzi kulingana na malengo ya ujifunzaji.

Nadharia ya Utibia ni mwafaka katika kuongoza utafiti huu kwa kuwa humsadia mwanafunzi katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Nadharia hii ilitusaidia kuelewa jinsi asili ya Kinyarwanda inavyoweza kuathiri njia za kujifunza na kufundisha Kiswahili na kuwawezesha walimu kuelewa vizuri mahitaji ya wanafunzi wenyе asili ya Kinyarwanda. Hii ni pamoja kuelewa changamoto wanazoweza kukabiliana nazo katika kujifunza Kiswahili. Nadharia hii imetusaidia kufahamu mazingira na muktadha wa darasa. Kwa hivyo, imewezesha kuelewa jinsi mwanafunzi anayejifunza Kiswahili kama lugha ya pili kutoka katika mazingira ya Kinyarwanda inavyoweza kumsadia mwalimu kuunda mikakati sahihi ya ufundishaji.

4.0. Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa Kinyarwanda kina athari kubwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kwa kuwa kuna mwingiliano wa karibu kati ya lugha hizi. Hivyo basi, utafiti umebaini kuwa wanafunzi wa Kiswahili hufanya

makosa ya kiothografia pale wanapoathiriwa na mtindo wa Kinyarwanda katika kuandika Kiswahili. Vilevile, kuna maneno ya Kinyarwanda ambayo hukaribiana na ya Kiswahili kimamatshi lakini hutofautiana kimaana. Aidha, maneno hayo huwa na maana tofauti na ile ya Kinyarwanda. Hali hii huwafanya wanafunzi kuchanganya maneno hayo na kudhani kuwa ni yenye maana sawa kama ilivyo katika lugha ya Kinyarwanda.

4.1. Athari za Lugha ya Kwanza kwa Lugha ya Pili

Data za utafiti zinaonesha kuwa wanafunzi hukumbwa na mwingiliano wa Kinyarwanda na Kiswahili. Mwingiliano huo hujitokeza kwenye baadhi ya maneno ya Kiswahili ambayo hukaribiana kimamatshi na yale ya Kinyarwanda. Mwalimu mmoja wa Kiswahili alithibitisha hayo akisema:

Ninakumbwa na mwingiliano wa kilugha. Pia, kuna ulinganifu wa Kinyarwanda na Kiswahili. Yaani, wanafunzi wetu hulinganisha vipengele vya Kinyarwanda na vile vya Kiswahili. Vipengele hivyo ni pamoja na matamshi na maandishi ya baadhi ya maneno. Yaani kuna maneno yenye mfanano wa kisemantiki na hata ule wa kimamatshi vya karibu kutoka Kinyarwanda kwenda Kiswahili. Kwa mfano: umurima (Kinyarwanda), mlima (Kiswahili), icyumba (Kinyarwanda), chumba (Kiswahili). Hivyo, husababishia wanafunzi kuathiriwa na Kinyarwanda wanaposoma Kiswahili

Chanzo: Mwalimu wa Kiswahili kutoka shule A

Data hiyo inaonesha kuwa wanafunzi wa Kiswahili wanakabiliwa na mwingiliano wa Kinyarwanda na Kiswahili. Mwingilano huo unasababishwa na matumizi ya kila siku ya Kinyarwanda katika shughuli za kibinadamu. Pia, athari nyingine ya Kinyarwanda kwa Kiswahili husababishwa na ulinganifu wa baadhi ya vipengele vya Kinyarwanda na vile vya Kiswahili. Maudhui ya data hii yanaoanishwa na mawazo ya Al-Khresheh (2015) ambaye hubainisha kuwa mwingiliano wa kilugha huathiri sana ujifunzaji wa lugha ya pili.

Athari hizo hutokea kwa kuwa wanafunzi wanajifunza lugha ya pili wakiwa na maarifa ya awali katika lugha yao ya kwanza. Mwalimu mwingine kutoka shule nyingine iliyohusishwa na utafiti huu alidhihirisha maoni yake akisema:

Mimi ninakabiliwa na athari ya kimaandishi kuhusu lugha ya kwanza kwa lugha ya pili. Yaani, wanafunzi wa Kinyarwanda huathiriwa sana na Kinyarwanda wakiandika Kiswahili. Kwa mfano, wanapoandika maneno ya Kiswahili yenye mfuatano wa konsonanti, wanapachika u ndani ya

mfuatano wa sauti husika. Kwa mfano, maneno mpanga, mpira na mlezi huandikwa na wanafunzi, kama ifuatayo: mupanga, mupira, mlezi.

Chanzo: Mwalimu wa Kiswahili kutoka shule B

Data hii inaonesha kuwa walimu wa Kiswahili wanakabiliwa na changamoto ya athari za kimaandishi za lugha ya Kinyarwanda wanapofundisha Kiswahili. Athari hii hujitokeza wakati wanafunzi wanapoandika maneno ya Kiswahili. Wanafunzi hao hujaribu kuandika maneno hayo kama yanavyotamkwa katika lugha yao ya kwanza. Athari hiyo inahusishwa na mawazo ya Niyomugabo (2016) ambaye anasema kuwa wanafunzi wanaosoma Kiswahili huathiriwa sana kimaandishi na lugha zao za kwanza. Hii inamaanisha kwamba wanapoandika kwa Kiswahili, hujaribu kuandika kama wanavyoandika lugha zao za kwanza. Lifuatalo ni dondo la mahojiano yaliyofanywa kwa mwalimu kutoka shule Ch.

Sisi walimu wa Kiswahili, tunakabiliwa na athari za kisemantiki za Kinyarwanda katika ujifunzaji wa Kiswahili. Yaani wanafunzi wetu wanachanganya maana za maneno ya Kiswahili na yale ya Kinyarwanda. Kwa mfano, ukisema neno la Kiswahili matakao, anasikia amatako ambalo kwa Kinyarwanda, ambayo humaanisha mapaja). Pia, akisema neno mhogo (Kiswahili) anasikia neno la Kinyarwanda umuhogo wenye maana ya koo.

Chanzo: Mwalimu wa Kiswahili kutoka shule Ch

Data hii inaonesha kuwa walimu wa Kinyarwanda wanakabiliwa na changamoto ya kutamka maneno na maana zake wakati wa ufundishaji wa Kiswahili. Wanafunzi wa Kinyarwanda wanachanganya maana za maneno ya Kiswahili na ya Kinyarwanda. Haya hufanyika kwa kuwa lugha hizi zinakaribiana moja kwa moja katika vipashio vyake kadhaa. Athari hii inaoanishwa na maoni ya Kemunto (2017) anayesema kuwa mtu anapovunja sheria za lugha, huenda akafanya makosa ya kisemantiki, yaani maana ya neno ama sentensi hubadilika na kupoteza maana yake ya asili.

4.2 Makosa ya Kiorthografia

Data za utafiti zinaonesha kuwa wanafunzi wa Kinyarwanda walifanya makosa ya kiuandishi walipojifunza lugha ya Kiswahili. Makosa hayo yalidhihirika kwenye uandishi wa maneno ya Kiswahili yaliyotolewa kwenye mazoezi ya imla. Jedwali lifuatalo linaonesha makosa hayo ya kiorthografia ambayo hufanywa na wanafunzi wa Kiswahili:

Jedwali Na. 1: Makosa ya Kiothografia ya Wanafunzi

| Shule | Wanafunzi | Asilimia (%) | Maneno ya Kinyarwanda | Maneno ya Kiswahili | Maneno yenyeye Makosa | Maneno Sahihi |
|--------------|-----------|--------------|-------------------------|----------------------|------------------------|----------------------|
| Shule A | 8 | 44.44 | <i>umuhogo umurima</i> | <i>mhogo mlima</i> | <i>muhogo mulima</i> | <i>mhogo mlima</i> |
| Shule B | 6 | 33.33 | <i>umupira umucanga</i> | <i>mpira mchanga</i> | <i>mupira muchanga</i> | <i>mpira mchanga</i> |
| Shule Ch | 4 | 22.22 | <i>umukondo umuzimu</i> | <i>mkondo mzimu</i> | <i>mukondo muzimu</i> | <i>mkondo mzimu</i> |
| Jumla | 18 | 100 | | | | |

Chanzo: Uwandani (2023)

Data katika Jedwali Na. 1 zinaonesha kuwa asilimia 44.44 ya wanafunzi wa Kinyarwanda wameathiriwa na mtindo wa kimaandishi wa lugha ya Kinyarwanda wanapoandika maneno ya Kiswahili. Kwa mfano, wanaandika neno ‘mhogo’ huku wakipachika sauti /u/ katikati ya sauti /m/ na sauti /h/. Pia, wanaandika neno ‘mlima’ kwa namna isiyo sahihi. Neno hilo liliandikwa kwa kupachika sauti /u/ katikati ya sauti /m/ na sauti /l/. Pia, asilimia 33.33 ya wanafunzi wa Kinyarwanda wanaathiriwa na lugha yao ya kwanza wanapoandika maneno ya Kiswahili yenyeye mfuatano wa konsonanti ‘mp’ na ‘mch’. Kwa mfano, wanapoandika maneno ‘mpira’ na ‘mchanga’, wanapachika sauti /u/ katikati ya sauti /m/ na sauti /p/. Pia, sauti /u/ hupachikwa katikati ya sauti /m/ na sauti /ch/. Vilevile, asilimia 22.22 ya wanafunzi wa Kinyarwanda waliandika vibaya maneno *mkondo* na *mzimu*. Haya, yaliandikwa kwa kupachika sauti /u/ baina ya sauti /m/ na sauti /k/. Pia, sauti /u/ ilipachikwa baina ya sauti m na sauti /k/.

4.3 Makosa ya Kimatamshi

Data za utafiti zilidhihirisha kuwa wanafunzi kutoka shule tatu za sekondari wilayani Gakenke wanafanya makosa ya kimatamshi wanaposoma baadhi ya maneno ya Kiswahili. Maneno hayo yalikuwa na mfanano wa moja kwa moja na maneno ya Kinyarwanda. Jedwali linalofuata linaonesha makosa yaliyodhihirika katika matamshi ya wanafunzi wa Kiswahili:

Jedwali Na. 2: Makosa ya Kimatamshi ya Wanafunzi wa Kiswahili

| Shule | Wanafunzi | Asilimia (%) | Maneno ya Kinyarwanda | Maneno ya Kiswahili | Hali ya Matamshi |
|--------------|-----------|--------------|-----------------------|---------------------|--------------------------------------|
| Shule A | 7 | 33.88 | <i>ikibiriti</i> | kiberiti | Matamshi ya sauti /k/ ya Kinyarwanda |
| Shule B | 6 | 33.33 | <i>ibendera</i> | bendera | Matamshi ya sauti /b/ ya Kinyarwanda |
| Shule Ch | 5 | 27.77 | <i>ijisho</i> | jicho | Matamshi ya sauti /j/ ya Kinyarwanda |
| Jumla | 18 | 100 | | | |

Chanzo: Uwandani (2023)

Jedwali Na. 2 hapo juu linadhihirisha kuwa wanafunzi wa Kinyarwanda wanaathiriwa na matamshi ya Kinyarwanda wakitamka baadhi ya maneno ya Kiswahili. Hili linajitokeza kwa sababu maneno ya Kiswahili yana muundo unaokaribiana na ule wa Kinyarwanda. Pia, sauti zinazounda maneno hayo zinafanana na zile za Kinyarwanda lakini matamshi yake ni tofauti. Kwa hiyo, asilimia 33.88 ya wanafunzi wa Kinyarwanda wametamka neno la Kiswahili /kiberiti/ kama wanavyotamka neno la Kinyarwanda /ikibiriti/ lenye maana sawa na neno la Kiswahili *kiberiti*.

Aidha, asilimia 33.33 ya wanafunzi wa Kinyarwanda wanatamka neno la Kiswahili /bendera/ kama wanavyotamka neno la Kinyarwanda /ibendera/ lenye maana sawa na neno *bendera* la Kiswahili. Vilevile, asilimia 27.77 ya wanafunzi wa Kinyarwanda wanatamka neno la Kiswahili /jicho/ kama wanavyotamka neno la Kinyarwanda /ijisho/ lenye maana ya *jicho* kwa Kiswahili.

4.4 Makosa ya Kisemantiki

Data za utafiti zinaonesha kuwa wanafunzi kutoka shule tatu teule walifanya makosa ya kimaana. Makosa hayo yalifanya kwa kuwa wanafunzi wa Kinyarwanda waliathiriwa na Kinyarwanda, yaani walichanganya maana za maneno ya Kiswahili kwa sababu maneno hayo yalikuwa yakifanana na maneno ya Kinyarwanda kimatamshi na hata kimaandishi. Maelezo haya yameoneshwa kwenye Jedwali Na. 3 lifualalo:

Jedwali Na. 3: Makosa ya Kisemantiki kwa Wanafunzi

| Shule | Wanafunzi | Asilimia % | Maneno ya Kinyarwanda | Maneno ya Kiswahili | Maana za Maneno |
|--------------|------------------|-------------------|------------------------------|----------------------------|---|
| Shule A | 8 | 44.44 | <i>amatako</i> | matako | Neno la Kinyarwanda /amatako/ linamaanisha <i>mapaja</i> kwa Kiswahili ilhali neno /matako/ la Kiswahili lina maana ya sehemu ya nyuma ya binadamu inakayoliwa. |
| Shule B | 5 | 27.77 | <i>amadini</i> | madini | Neno la Kinyarwanda /amadini/ linamaanisha dini kwa Kiswahili ilhali /madini/ kwa Kiswahili ni mawe yenze thamani kubwa yanayochimbwa udongoni. |
| Shule Ch | 5 | 27.77 | <i>ikiremba</i> | ilemba | Neno la Kinyarwanda /ikiremba/ linamaanisha mwanamume ambaye hana nguvu za kiume pamoja na uwezo wa kutozaa ilhali neno /kilemba/ kwa Kiswahili linamaanisha kitambaa kinachovaliwa kichwani. |
| Jumla | 18 | 100 | | | |

Chanzo: Uwandani (2023)

Data katika Jedwali Namba 3 zinaonesha kuwa asilimia 44.44 ya wanafunzi wa Kinyarwanda wanaathiriwa na Kinyarwanda wanapotofautisha maana za maneno. Kwa mfano, neno la Kinyarwanda /amatako/ na la Kiswahili /matako/. Kwa hiyo, asilimia 27.77 ya wanafunzi wa Kinyarwanda wanaathiriwa pia na lugha yao ya kwanza, yaani wanachanganya maana ya neno la Kinyarwanda /amadini/ na lile la Kiswahili /madini/. Hatimaye, asilimia 27.77 ya wanafunzi wa Kinyarwanda wanachanganya maana ya neno la Kinyarwanda /ikiremba/ na lile la Kiswahili /kilemba/. Kwa jumla, shule A inaonesha kiwango cha juu cha makosa, wakati shule B na Ch zina asilimia sawa ya makosa, zikonesha haja ya mafunzo ya ziada kuhusu matumizi sahihi ya maneno na maana yao katika lugha hizi mbili.

5.0 Hitimisho na Mapendekazo

Makala hii imejishughulisha na athari za lugha ya kwanza kwa lugha ya pili. Lengo lilikuwa kuchunguza athari za Kinyarwanda katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kwa kutumia mifano kutoka shule za sekondari za wilaya ya Gakenke. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa wanafunzi wanaathiriwa na lugha ya Kinyarwanda kimatamshi na hata kimaandishi. Kwa hivyo, mwingiliano wa lugha unajitokeza. Kwa ujumla, wanafunzi wa lugha ya pili huathiriwa na lugha ya kwanza.

Haya hujitokeza kwa kuwa wanatumia lugha za kigeni wakiwa shulenii tu. Wanapofika nyumbani huathiriwa na mazingira ambamo hutumia Kinyarwanda. Kwa hiyo, makala hii inapendekeza yafuatayo: mosi, Wizara ya Elimu inapaswa kuanzisha mafunzo maalumu kwa walimu ili kuwapa mbinu bora za kufundisha Kiswahili kwa wanafunzi wenye asili ya Kinyarwanda. Pili, Bodi ya Elimu Rwanda inapaswa kuboresha mtaala ili kujumuisha mikakati inayokabiliana na athari za lugha mbili. Tatu, viongozi wa shule wanapaswa kuanzisha vipindi nya ziada nya Kiswahili na kuhimiza matumizi ya Kiswahili nje ya darasa. Nne, walimu wanahitaji kutumia mbinu shirikishi na ubunifu, kama vile kutumia teknolojia na programu za kubadilishana wanafunzi. Mwisho, wanafunzi wanapaswa kuhamasishwa kushiriki kikamilifu katika klabu za Kiswahili na miradi ya kijamii ili kuboresha ustadi wao wa lugha. Kwa pamoja, juhudii hizi zinaweza kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari, huku zikikabiliana na athari za Kinyarwanda.

Marejeleo

- Al-Khresheh, M.H. (2015). “A Review Study of Interlanguage Theory.” *International Journal of Applied Linguistics and English Literature*. 4(3): 123-131.
- Bichwa, S. na Mwendamseke, F. (2021). “Ufaafu wa Matumizi ya Nadharia ya Utibia katika Mbinu za Kufundia Lugha ya Kigeni.” *Kioo cha Lugha*. 19(2): 92-102.
- Debyser, F. (1970). “La linguistique Contrastive et les Interférences.” *Langue Française*. 8(1): 34-35.
- Ellis, R. (1995). “A Theory of Instructed Second Language Acquisition”. Katika N. Ellis (Mh.), *Implicit and Explicit Learning of Languages*. Academic Press. Kur. 1-13
- Fromkin, V., Rodman, R. na Hyams, N. (2007). “An Introduction to Language (Toleo la 8.)”. Boston: Thomson Wadsworth.
- Kemunto, A.B. (2017). “Makosa ya Kisemantiki katika Mawasiliano Andishi ya Kiswahili ya Wanafunzi wa Shule za Shule za Upili Nchini Kenya”. *International Arts Journal and Education*. 1(2):13-24.
- Komunte, B.S. (2001). “The Impact of Bantu Languages in English Language Learning Processes in Tanzania Secondary Schools”. *Makala ya Kongamano la Kimataifa Kiswahili*, 2000, Kur. 287 – 296.
- Maho, J.F. (2009). NUG Online: The online Version of the New Updated Guthrie List, A Referential Classification of the Bantu Language. Version dated June 4th 2009. Inapatikana katika <https://rb.gy/saydzj>. Ilisomwa tarehe 25 Machi 2023.

- Maho, J.P. (2009). The Online Version of the New Updated Guthrie List: A Referential Classification of the Bantu Languages. NUGL Online. <https://shorturl.at/bjz35>
- Mлага, W. (2017). “Historia ya Kiswahili Nchini Rwanda: Kielelezo cha Nafasi ya Utashi wa Kisiasa katika Ustawi wa Lugha ya Kiswahili”. *Kioo cha Lugha*. 15(1): 1-19.
- Ngugi, J.K. (2007). Uchunguzi wa Taathari za Kifonolojia mionganoni mwa Wanafunzi Wagikuyu: Mfano kutoka Tarafa ya Bahati, Nakuru. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Egerton.
- Niyomugabo, C. (2016). “Ufundishaji wa Kiswahili katika Shule za Rwanda: Historia Tathmini ya Makosa, Matatizo na Mahitaji”. *KISWAHILI*. 79(3): 79-92.
- Ntawiyanga, S. (2020). “Makosa ya Upatanishi wa Kisarufi katika Ujifunzaji Lugha ya Pili: Mfano wa Wanafunzi wa Kiswahili katika Shule za Upili Wilayani Muhangi, Nchini Rwanda”. *Kioo cha Lugha*. 17(3): 17-32.
- Ontieri, J.O. (2010). Uchanganuzi wa Makosa katika Insha za Wanafunzi wa Shule za Upili: Mfano wa Wilaya ya Nakuru, Kenya. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Cha Egerton.
- Ontieri, J.O. (2017). “Athari za Kifonolojia za Lugha ya Kwanza katika Kiswahili: Mfano wa Lugha Teule za Kibantu Nchini Kenya”. *MULIKA*. 34(12):1-13. <https://shorturl.at/psw06>. Ilisomwa tarehe 7 Februari 2024.
- Ponera, A. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasnifu* (Toleo la 1). Dodoma: Central Tanganyika Press.
- Richards, J.C. (1974). “Error Analysis and Second Language Strategies”. Katika J.H. Schumann and N. Stenson (Wah.), *New Frontiers in Second Language Learning*. Rowley, Mass.: Newbury House. Kur. 1-27.